**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

# MKOA WA KATAVI




## TAARIFA YA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI MKOA WA KATAVI MWAKA 2021 HADI JUNI, 2025 NA SHUGHULI ZITAKAZOTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

# YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ..... 1

1.1 Eneo la Mkoa ..... 1

1.2 Maeneo ya Kiutawala ..... 1

1.3 Idadi ya Watu ..... 1

1.4 Majukumu Makuu ya Sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ..... 1

2.0. SEKTA YA UWEKEZAJI ..... 2

2.1 Wilaya ya Tanganyika ..... 2

2.2Wilaya ya Mpanda ..... 3

2.3Wilaya ya Mlele ..... 4

2.4Eneo la Uwekezaji SIDO ..... 4

3.0 SEKTA YA VIWANDA ..... 5

4.0SEKTA YA BIASHARA ..... 8

4.1Mamlaka ya Serikali za Mitaa ..... 8

5.1Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ..... 12

6.1Wakala wa Vipimo (WMA) ..... 13

7.1SEKTA YA BANDARI ..... 14

8.1SEKTA YA USAFIRI WA ANGA ..... 15

9.1SEKTA YA MADINI ..... 16

10.1SHIRIKA LA VIWANGO (TBS) ..... 19

11.1HITIMISHO ..... 19

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Eneo la Mkoa

Mkoa wa Katavi ulianzishwa rasmi tarehe 01 Machi, 2012 kupitia tangazo la serikali Na. 72. Mkoa una ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 47,527 ambapo eneo la nchi kavu ni kilomita za mraba 45,843 na eneo la maji ni kilomita za mraba 1,684. Katika eneo la nchi kavu eneo lifaalo kwa Kilimo ni Hekta 932,136 na eneo la misitu ni Hekta 3,142,232.

### 1.2 Maeneo ya Kiutawala

Mkoa una jumla ya Wilaya tatu (3) ambazo ni Wilaya ya Mpanda, Mlele na Tanganyika. Halmashauri zipo tano (5) ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe. Tarafa zipo 10, Kata 58, Vijiji 172, Mitaa 43 na vitongoji 931.

### 1.3 Idadi ya Watu

Kwa mwaka 2025 Mkoa wa Katavi unakisiwa kuwa na jumla ya watu 1,254,996 ikiwa wanaume ni 622,919 na wanawake ni 632,077. Hivyo ikadariwa wakazi 102,038 wameongezeka baada ya sensa ya mwaka 2022 ambapo matokeo ya sensa yanaonyesha Mkoa wa Katavi unajumla ya watu 1,152,958.

### 1.4 Majukumu Makuu ya Sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

Majukumu makuu ya sehemu ya viwanda, biashara na uwekezaji ni pamoja na kusimamia, kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili kukuza na kuendeleza maendeleo ya viwanda, biashara na uwekezaji ndani ya Mkoa.

## 2.0. SEKTA YA UWEKEZAJI

Mkoa wa Katavi umebarikiwa kuwa na fursa nyingi za uwekezaji, baadhi ya fursa hizi ni uwepo wa ardhi yenye rutuba kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji, uwepo wa madini ya aina mbalimbali, uwepo wa vivutio vingi vya utalii hasa kutokana na uwepo wa hifadhi ya Taifa ya Katavi. Pia fursa ya uwepo wa ziwa Tanganyika kwa ajili ya uwekezaji kwenye uvuvi na vyombo vya usafiri, fursa ya uwepo wa bandari ya Karema ambayo ni ya kisasa, fursa za uanzishaji wa viwanda mbalimbali kama vile viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo, viwanda vya mabati, vinywaji, sementi nk. Ili kuhamasisha na kuvutia wawekezaji, Mkoa wa Katavi umetenga maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uwekezaji kama ifuatavyo;

### 2.1 Wilaya ya Tanganyika

i. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika imetenga ekari 115,000 katika eneo la Luhafwe kwa ajili ya uwekezaji kwenye kilimo na viwanda. Ekari zilizopata wawekezaji ni 56,479, ambapo jumla ya wawekezaji 26 wapo katika hatua mbalimbali za kuanza uwekezaji. Baadhi ya wawekezaji wakubwa waliomilikishwa ardhi na wapo katika hatua za awali za uwekezaji ni SEEDLAND, MERU AGRO TOUR CONSULTANT LTD na ASA. Aidha, jumla ya ekari 58,521 zimetengwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama makazi na hifadhi ya misitu.

ii. Halmashauri imetenga eneo la ekari 30 katika kijiji cha Kabungu ambapo zitatumika katika uwekezaji wa viwanda.

iii. Pia zipo ekari 3,160 za watu binafsi ambazo mwekezaji anaweza kuingia kwenye makubalino na wenye maeneo hayo.

Mchanganuo wa ardhi kwa ajili matumizi ya uwekezaji na matumizi mengine umeoneshwa katika jedwali lifuatalo;

| Ekari zilizotengwa | Umiliki wa Eneo | | Ekari zilizopata wawekezaji | Ekari zilizotengwa kwa matumizi mengine | Ekari ambazo hazijapata wawekezaji | Idadi ya wawekezaji waliofanya uwekezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Watu Binafsi | | | | |
| 115,000 | 115,000 | 3,160 | 56,479 | 58,521 | 3,160 watu binafsi | 26 |

Chanzo cha takwimu ni Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri 2024/2025.

## 2.2 Wilaya ya Mpanda

Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ambazo zipo katika Wilaya ya Mpanda zimetenga maeneo ya uwekezaji kama ifuatavyo;

- ✓ Ekari 3,020 zimetengwa eneo la Nsemulwa kwa ajili ya uwekezaji kwenye viwanda.
- ✓ Ekari 2,648.25 zimetengwa eneo la Shanwe kwa ajili ya vyuo.
- ✓ Eneo la mlima wa Kijiji cha Makongoro limetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa kiwanda cha sementi.
- ✓ Zipo ekari 13 eneo la Msangama kwa ajili ya uchimbaji wa madini na uanzishaji wa viwanda vya kuchakata madini.
- ✓ Ekari 115 zimetengwa Kijiji cha Mtapenda Halmashauri ya Nsimbo kwa ajili ya uwekezaji kwenye viwanda.

Mchanganuo wa ardhi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji umeoneshwa katika jedwali lifuatalo;

| Ekari zilizotengwa | Umiliki wa Eneo | | Ekari zilizopata wawekezaji | Ekari ambazo hazijapata wawekezaji | Idadi ya wawekezaji waliofanya uwekezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Watu Binafsi | | | |
| 7,161.72 | 1,056.47 | 6,031 | 470.47 | 6,617 | 4 |

Chanzo cha takwimu ni Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri 2024/2025.

### 2.3 Wilaya ya Mlele

Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe ambazo zipo katika Wilaya ya Mlele zimetenga maeneo ya uwekezaji kama ifuatavyo;

- ✓ Ekari 20 zimetengwa eneo la Inyonga Halmashauri ya Mlele kwa ajili ya uwekezaji kwenye viwanda.
- ✓ Ekari 120.72 zimetengwa eneo la Majimoto na Usevya kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo.
- ✓ Ekari 51.25 zimetengwa eneo la Kitupa - Majimoto na Usevya kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali katika sekta ya biashara.
- ✓ Ekari 26.37 zimetengwa eneo la Majimoto na Usevya kwa ajili ya uwekezaji mbalimbali katika sekta za Elimu na Afya.

Mchanganuo wa ardhi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji umeoneshwa katika jedwali lifuatalo;

| Ekari zilizotengwa | Umiliki wa Eneo | | Ekari zilizopata wawekezaji | Ekari ambazo hazijapata wawekezaji | Idadi ya wawekezaji waliofanya uwekezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Watu Binafsi | | | |
| 218.34 | 108.43 | 110 | 110 | 88.43 | 103 |

Chanzo cha takwimu ni Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri 2024/2025.

### 2.4 Eneo la Uwekezaji SIDO

SIDO Mkoa wa Katavi imetenga eneo la ekari 21 kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vya aina mbalimbali. Pia SIDO inamajengo yanayokodishwa kwa ajili ya viwanda vidogo na chumba cha baridi (coldroom) kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa. Wawekezaji wanakaribishwa kwa ajili ya kuingia makubaliano ya kuwekeza kwenye eneo na majengo ya SIDO.

## 3.0 SEKTA YA VIWANDA

Idadi ya viwanda katika Mkoa wa Katavi imeongezeka kutoka 873 mwaka 2021 hadi 1,906 mwezi Juni, 2025. Kati ya viwanda hivyo viwanda vikubwa ni 6, viwanda vya kati ni 22, viwanda vidogo ni 541, na viwanda vidogo sana ni 1,334, jumla ya watu walioajiriwa katika viwanda hivyo ni 6,212. Mchanganuo wa viwanda hivi umechanganuliwa Kihalmashauri katika jedwali lifuatavyo;

**Jedwali la Orodha ya Viwanda vilivyopo katika Halmashauri hadi Juni, 2025**

| Jina la Halmashauri | Kundi la Kiwanda | Idadi ya Wafanyakazi | Mtaji Uliowekezwa katika Mitambo (TSH | Idadi ya Viwanda vilivyopo hadi sasa | Idadi ya walioajiriwa katika Viwanda |
|---|---|---|---|---|---|
| MPANDA MC | Kiwanda Kidogo Sana *(Micro Enterprise)* | 1 – 4 | hadi milioni 5 | 470 | 1,802 |
| | Kiwanda Kidogo *(Small Enterprise)* | 5 – 49 | Milioni 5 hadi milioni 200 | 62 | 501 |
| | Kiwanda cha Kati *(Medium Enterprise)* | 50 – 99 | Milioni 200 hadi milioni 800 | 7 | 41 |
| | Kiwanda Kikubwa *(Large Enterprise)* | Zaidi ya 100 | Zaidi ya milioni 800 | 2 | 86 |
| **Jumla Ndogo** | | | | **541** | **2,430** |
| | | | | | |
| NSIMBO DC | Kiwanda Kidogo Sana *(Micro Enterprise)* | 1 – 4 | hadi milioni 5 | 228 | 460 |
| | Kiwanda Kidogo *(Small Enterprise)* | 5 – 49 | Milioni 5 hadi milioni 200 | 126 | 248 |
| | Kiwanda cha Kati *(Medium Enterprise)* | 50 – 99 | Milioni 200 hadi milioni 800 | 3 | 29 |

| Jina la Halmashauri | Kundi la Kiwanda | Idadi ya Wafanyakazi | Mtaji Uliowekezwa katika Mitambo (TSH | Idadi ya Viwanda vilivyopo hadi sasa | Idadi ya walioajiriwa katika Viwanda |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kiwanda Kikubwa *(Large Enterprise)* | Zaidi ya 100 | Zaidi ya milioni 800 | 2 | 235 |
| **Jumla Ndogo** | | | | **359** | **972** |
| | | | | | |
| TANGANYIKA DC | Kiwanda Kidogo Sana *(Micro Enterprise)* | 1 – 4 | hadi milioni 5 | 321 | 685 |
| | Kiwanda Kidogo *(Small Enterprise)* | 5 – 49 | Milioni 5 hadi milioni 200 | 281 | 552 |
| | Kiwanda cha Kati *(Medium Enterprise)* | 50 – 99 | Milioni 200 hadi milioni 800 | 3 | 82 |
| | Kiwanda Kikubwa *(Large Enterprise)* | Zaidi ya 100 | Zaidi ya milioni 800 | 1 | 59 |
| **Jumla Ndogo** | | | | **606** | **1,378** |
| | | | | | |
| MLELE DC | Kiwanda Kidogo Sana *(Micro Enterprise)* | 1 – 4 | hadi milioni 5 | 146 | 358 |
| | Kiwanda Kidogo *(Small Enterprise)* | 5 – 49 | Milioni 5 hadi milioni 200 | 31 | 227 |
| | Kiwanda cha Kati *(Medium Enterprise)* | 50 – 99 | Milioni 200 hadi milioni 800 | 0 | 0 |
| | Kiwanda Kikubwa *(Large Enterprise)* | Zaidi ya 100 | Zaidi ya milioni 800 | 0 | 0 |
| **Jumla Ndogo** | | | | **177** | **585** |
| | | | | | |

| Jina la Halmashauri | Kundi la Kiwanda | Idadi ya Wafanyakazi | Mtaji Uliowekezwa katika Mitambo (TSH | Idadi ya Viwanda vilivyopo hadi sasa | Idadi ya walioajiriwa katika Viwanda |
|---|---|---|---|---|---|
| MPIMBWE DC | Kiwanda Kidogo Sana *(Micro Enterprise)* | 1 – 4 | hadi milioni 5 | 166 | 191 |
| | Kiwanda Kidogo *(Small Enterprise)* | 5 – 49 | Milioni 5 hadi milioni 200 | 47 | 276 |
| | Kiwanda cha Kati *(Medium Enterprise)* | 50 – 99 | Milioni 200 hadi milioni 800 | 9 | 310 |
| | Kiwanda Kikubwa *(Large Enterprise)* | Zaidi ya 100 | Zaidi ya milioni 800 | 1 | 70 |
| **Jumla Ndogo** | | | | **223** | **847** |
| **JUMLA KUU** | | | | **1,906** | **6,212** |

***Muhimu:*** *Endapo kigezo cha mtaji kitakuwa kikubwa kuliko idadi ya wafanyakazi, basi kigezo cha mtaji kitatumika kutafsiri aina ya kiwanda.*



*Kiwanda cha kuchambua Pamba Katavi*

# 4.0 SEKTA YA BIASHARA

## 4.1 Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Kwa mujibu wa ikama mahitaji ya watumishi wa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa Mkoa wa Katavi ni 45 watumishi waliopo ni 15 upungufu ni 30 hii ikiwa ni asilimia 33 ya watumishi waliopo. Mchanganuo wa watumishi katika Halmashauri umeonyeshwa katika jedwali hapa chini.

| Jina la Halmashauri | Mahitaji | Waliopo | Upungufu | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Mpanda MC | 9 | 3 | 6 | 33 |
| Nsimbo DC | 9 | 3 | 6 | 33 |
| Mlele DC | 9 | 2 | 7 | 22 |
| Mpimbwe DC | 9 | 4 | 5 | 44 |
| Tanganyika DC | 9 | 3 | 6 | 33 |
| **JUMLA** | **45** | **15** | **30** | **33** |

### 4.1.1 Idadi ya Wafanyabiashara na Makusanyo ya Mapato mwaka 2021 hadi Juni 2025

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Juni, 2025 idadi ya wafanyabiashara walipa kodi imeongezeka toka 5,518 mwaka 2021 hadi 8,124 Juni 2025 sawa na ongezeko la asilimia 47. Aidha, kiasi cha fedha kilichokusanywa kutokana na shughuli za biashara kimeongezeka toka Tshs. 3,091,563,715.23 mwaka, 2021 hadi Tshs,4,764,467,509.11 mwezi Juni, 2025. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 54. Jedwali hapa chini limechanganua kwa kila Halmashauri kama ifuatavyo;

| Jina la Halmashauri | Idadi ya Wafanyabiashara mwaka 2021 | Idadi ya Wafanyabiashara hadi Juni 2025 | % Ongozeko la wafanyabiashara | Fedha zilizokusanywa mwaka 2021 | Fedha zilizokusanywa hadi Juni 2025 | % Ongozeko la Makusanyo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mpanda MC | 1,755 | 2,290 | 30 | 2,659,540,188.49 | 3,896,308,390.11 | 47 |
| Nsimbo DC | 1,157 | 1,563 | 33.2 | 291,691,026.74 | 359,265,142.00 | 23.16 |
| Tanganyika DC | 1,853 | 2,252 | 21.5 | 78,000,000.00 | 299,099,127.00 | 384 |
| Mlele DC | 426 | 1,096 | 157 | 35,148,500.00 | 135,334,500.00 | 285 |
| Mpimbwe DC | 327 | 923 | 179 | 27,184,000.00 | 74,460,350.00 | 174 |
| **JUMLA** | **5,518** | **8,124** | **47** | **3,091,563,715.23** | **4,764,467,509.11** | **54** |

### 4.1.2 Mchango wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mapato ya Halmashauri.

Katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji kupitia vyanzo mbalimbali imechangia kiasi Tshs. 2,068,714,940.39 katika makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri hii ikiwa ni asilimia 11.4 ya uchangiaji wa sekta katika makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Mchanganuo ni kama jedwali lifuatalo linavyochanganua;

| Jina la Halmashauri | Hali halisi ya makusanyo kwa mwaka 2024/25 | Kiasi kilichokusanywa kutoka vyanzo vya sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji hadi Juni, 2025 | % ya mapato yaliyokusanywa toka sekta viwanda, biashara na uwekezaji |
|---|---|---|---|
| Mpanda MC | 3,896,308,390.11 | 1,347,719,133.19 | 34.6 |
| Nsimbo DC | 2,396,568,200.00 | 77,390,740.00 | 3.2 |
| Tanganyika DC | 6,712,680,489.49 | 81,738,900.00 | 1.2 |
| Mlele DC | 2,005,000,000.00 | 99,847,140.00 | 5 |
| Mpimbwe DC | 3,064,352,588.42 | 462,019,027.20 | 15.1 |
| **JUMLA** | **18,074,909,668.02** | **2,068,714,940.39** | **11.4** |

### 4.1.3 Makisio ya Idadi ya Wafanyabiashara na Makusanyo ya Mapato kwa mwaka 2025/26

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi mwezi Juni, 2026 makisio ya wafanyabiashara watao ongezeka ni 1,064 ambayo ni sawa na asilimia 13 ya ongezeko ikilinganishwa na mwaka 2024/25. Aidha, makisio ya makusanyo ya fedha kutokana na ongezeko la wafanyabiashara ni Tshs. 796,376,067.19. Mchanganuo wa makisio haya ni kama unavyoonekana katika jedwali lifuatalo;

| Jina la Halmashauri | Idadi ya Wafanyabiashara hadi Juni 2025 | Makisio ya Wafanyabiashara watakao ongezeka hadi Juni 2026 | % Ongozeko la wafanyabiashara | Makisio ya mapato yatakayokusanywa kutokana na ongezeko la wafanyabiashara hadi Juni, 2026 |
|---|---|---|---|---|
| Mpanda MC | 2,290 | 400 | 17 | 100,000,000.00 |
| Nsimbo DC | 1,563 | 103 | 8 | 39,733, 542.00 |
| Tanganyika DC | 2,252 | 118 | 5 | 121,500,000.00 |
| Mlele DC | 1,096 | 106 | 10 | 41,910,000.00 |
| Mpimbwe DC | 923 | 337 | 37 | 632,966,067.19 |
| **JUMLA** | **8,124** | **1,064** | **13** | **796,376,067.19** |

### 4.1.4 Orodha ya vyanzo vipya vya mapato vitakavyoanzishwa mwaka 2025/26

Katika mwaka wa fedha 2025/26 wataalam wa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji kwa kushirikiana na wataalam wengine wamepanga kubuni na kuanzisha vyanzo vipya vya mapato kama ifuatavyo;

| S N | Jina la chanzo kipya cha mapato | Jina la Kata chanzo kipya kitapoanzishwa | Jina la Kijiji/Mtaa chanzo kipya kitapoanzishwa |
|---|---|---|---|
| **Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda** | | | |
| 1. | Ushuru wa maegesho | Kashaulili na Majengo | Kashaulili na Majengo |
| 2. | Kodi ya Vibanda | Mpanda Hotel | Mpanda Hotel |
| **Halmashauri ya Wilaya Mlele** | | | |
| **1.** | Stendi ya Malori | Inyonga | Inyonga |
| **Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe** | | | |
| 1 | Uuzaji wa tofali | Usevya - Kiwanda cha matofali | Usevya |
| 2 | Ushuru wa probox na basi | Usevya-stendi | Usevya |
| **Halmashauri ya Tanganyika** | | | |
| 1. | Leseni za wakandarasi wanaojenga barabara | Kata za Kabungu,Kasekese,Karema,Sibwesa na Tongwe | Kabungu,Kasekese,Karema, Sibwesa na Majalila |
| Halmashauri ya Nsimbo | | | |
| 1. | Standi ya mabasi NSIMBO | KAPALALA | Songambele |

## 5.1Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

### 5.1.1 Idadi ya Watumishi

Kwa mujibu wa ikama ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mahitaji ya watumishi wa TRA Mkoa wa Katavi ni **87** watumishi waliopo ni 62 upungufu ni 25 hii ikiwa ni asilimia **40** ya watumishi waliopo.

### 5.1.2Idadi ya Walipa kodi na Makusanyo

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Juni 2025, idadi ya walipakodi kupitia TRA Mkoa wa Katavi imeongezeka toka 8,125 mwaka 2021 hadi **15,634** kufikia Juni 2025. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia **192.42.** Makusanyo ya kodi yaliyokusanywa kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Juni 2025 ni shilingi **39,523,923,975.78** sawa na asilimia **104.67** ya lengo la kukusanya kiasi cha shilingi 21,766,675,068.97. Kumekuwa na ongezeko la asilimia **242.23** ukilinganisha na makusanyo kwa kipindi cha miaka minne ya nyuma.

### 5.1.3Makusanyo ya mapato kwa mwaka 2024/25 na Makisio ya mapato kwa mwaka 2025/26

Katika mwaka wa fedha 2024/25, TRA Mkoa wa Katavi ilikisia kukusanya kiasi cha shilingi **15,992,401,618.58** hadi mwezi Juni, 2025 kiasi kilichokusanywa ni shilingi

**18,846,311,972.27** sawa na asilimia **123.09** ya lengo. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2025/26, TRA Mkoa wa Katavi imekisia kukusanya kiasi cha shilingi **19,971,679,893.08** hii ikiwa ni ongezeko la asilimia **25.43** ikilinganishwa na makisio ya mwaka wa fedha wa 2024/25. Mchanganuo wa makisio haya ni kama unavyoonekana katika jedwali lifuatalo;

| Wilaya | Makusanyo kwa mwaka 2024/25 | Makisio ya mapato kwa mwaka 2025/26 | % Ongozeko la mapato |
|---|---|---|---|
| Mpanda | 11,604,850,932.00 | 13,410,106,048.32 | 25 |
| Tanganyika | 1,961,743,941.53 | 2,539,087,540.22 | 25 |
| Mlele | 3,156,951,044.94 | 4,022,486,303.29 | 25 |
| **JUMLA** | **16,723,545,919.11** | **19,971,679,891.83** | **25** |

## 6.1 Wakala wa Vipimo (WMA)

### 6.1.1Idadi ya Watumishi

Kwa mujibu wa ikama ya Wakala wa Vipimo (WMA) mahitaji ya watumishi wa WMA Mkoa wa Katavi ni 6 watumishi waliopo ni 6 upungufu ni 0 hii ikiwa ni asilimia 0 ya watumishi waliopo.

### 6.1.2 Utekelezaji wa Shughuli

Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi Juni, 2025 Wakala wa Vipimo Mkoa wa Katavi umefanya ukaguzi katika jumla ya vipimo 29,788 kati hivyo vipimo vilivyobainika kuwa na kasoro ni 1,241 kiasi cha fedha kilichokusanywa kutokana na faini na tozo mbalimbali toka mwaka 2021 hadi Juni, 2025 ni Tshs. 876,209,439.00. Aidha, vipimo vilivyofanyiwa ukaguzi kwa mwaka 2024/25 ni 9,014 kati ya hivyo vipimo vilivyobainika kuwa na kasoro ni 392 kiasi kilichokusanywa kutokana na faini na tozo ni Tshs. 231,773,438.00. Matokeo ya ukaguzi uliofanywa na Wakala wa Vipimo yamefanya wafanyabiashara wamekuwa na mwitikio wa kutumia vipimo sahihi.

### 6.1.3Shughuli zitakazotekelezwa mwaka 2025/26

Katika mwaka wa fedha wa 2025/26 Wakala wa Vipimo Mkoa wa Katavi unakusudia kufanya ukaguzi katika jumla ya vipimo **9,893** na kutoa elimu ya matumizi sahihi ya vipimo kwa wafanyabiashara wapatao **8,500** na kwa wananchi **720,000.**

Ofisi ya Wakala wa Vipimo Katavi itaendelea kufanya kaguzi mbalimbali na kutoa elimu ya matumizi ya vipimo sahihi kwa wananchi na wafanyabiashara.

## 7.1SEKTA YA BANDARI

### 7.1.1Idadi ya Watumishi

Kwa sasa Bandari ya Karema ina jumla ya watumishi wa umma 7.

### 7.1.2Utekelezaji wa Shughuli

Bandari ya Karema imeanza kutumika Septemba, 2022 tani zilizopitia bandari ya Karema hadi Juni, 2025 ni **tani 11,252** kiasi cha fedha kilichokusanywa ni **Tshs. 201,410,709.22.** Bidhaa zinazopitia bandari ya Karema kwa wingi ni mchele, unga, mahindi na makaa ya mawe.




*Bandari ya Karema*

### 7.1.3 Shughuli zitakazotekelezwa mwaka 2025/26

Katika mwaka wa fedha wa 2025/26 Mamlaka ya Bandari itaendelea kusimamia ujenzi wa meli za mizigo **nne (4).** Meli hizi zinajengwa na Kampuni ya Kichina iitwayo **Ankola Shipyard Co. Ltd** iliyoingia mkataba na TPA wa kujenga meli zenye uwezo wa kubeba **tani 2,000** kila moja. Ujenzi wa meli hizi unategemea kukamilika mwaka 2027. Shughuli nyingine zitakazofanyika ni usafirishaji wa madini kutoka DR Congo.

## 8.1 SEKTA YA USAFIRI WA ANGA

### 8.1.1 Idadi ya Watumishi

Kwa mujibu wa ikama watumishi wanaotakiwa katika uwanja wa ndege wa Mpanda ni 31 watumishi waliopo ni 22 upungufu ni 9 hii ikiwa ni asilimia 71 ya watumishi waliopo.

### 8.1.2Utekelezaji wa Shughuli

Huduma ya usafiri wa anga Mkoani Katavi ilianza kutolewa tarehe 26 Oktoba 2019, tangu kipindi hicho hadi Juni, 2025 idadi ya wasafiri imeongezeka kutoka 5,721 mwaka 2019 hadi 29,655 Juni, 2025. Idadi ya siku za kusafiri ni mara tatu kwa wiki yaani siku ya Jumanne, Alhamisi na Jumamosi. Kiasi cha fedha kilichokusanywa kimeongezeka toka Tshs.64,274,000.00 mwaka 2019 hadi Tshs. 236,450,000.00 Juni, 2025.



*Jengo la Uwanja wa ndege wa Mpanda*

### 8.1.3 Shughuli zitakazotekelezwa mwaka 2025/26

Katika mwaka wa fedha wa 2025/26 shughuli zilizopangwa kufanyika ni kuendelea na uendeshaji wa kiwanja na kutunza miundombinu yake.

## 9.1SEKTA YA MADINI

### 9.1.1 Idadi ya Watumishi

Kwa mujibu wa ikama watumishi wanaotakiwa katika Ofisi ya Afisa Madini Mkazi ni 22 watumishi waliopo ni 22 upungufu ni 0 hii ikiwa ni asilimia 100 ya watumishi waliopo.

### 9.1.2 Idadi ya Migodi

Mkoa wa Katavi umejaliwa kuwa na madini ya aina mbalimbali kama vile dhahabu, shaba, Galena, Fedha (Silver), Nickel, Mangenese nk. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Juni, 2025 ni kuongezeka kwa idadi ya migodi toka 911 mwaka 2021 hadi 1,600 Juni 2025, kati hiyo migodi mikubwa ni 0, migodi ya kati ni 16 na migodi midogo

ni 1,584 Idadi ya Watanzania waliojipatia ajira kutokana na shughuli za madini ni zaidi ya 15,000 wengine wana ajira ya kuduma na wengine wana ajira za mikataba.



Kiwanda cha kuchenjua madini cha Katavi Mining



Kiwanda cha kuchanjua madini cha Jema Jione

### 9.1.3 Soko la Madini la Mpanda

Soko la madini Mkoa wa Katavi lilianzishwa mwezi Mei, 2019 katika Manispaa ya Mpanda. Jumla ya mauzo ya dhahabu hadi Juni, 2025 ni gramu 1,514,363.17, gramu hizo zina thamani ya Tsh. 182,646,244,145.66. Aidha, mrabaha uliokusanywa ni Tsh. 10,617,479,995.43, ada ya ukaguzi *(clearing and inspection fee)* kiasi cha Tsh. 1,664,415,700.32 na ushuru wa huduma Tsh. 680,236,080.39 zilipelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya ya Nsimbo, Tanganyika na Manispaa ya Mpanda.

### 9.1.4 Biashara ya Makinikia

Tani za makinikia zilizosafirishwa nje ya nchi hadi Juni, 2025 ni tani 28,146.58 zikiwa na thamani ya Tsh. 205,040,715,532.77 ambapo Mrabaha wa Tsh. 12,300,660,331.44 ulikusanywa na ada ya ukaguzi Tsh. 2,050,114,013.69 ilikusanywa.

### 9.1.5 Makusanyo ya fedha yatokanayo na shughuli za madini

Makusanyo ya fedha yatokanayo na shughuli mbalimbali za madini yameongezeka mwaka hadi mwaka kama inavyoonyesha katika kwenye jedwali hapa chini.

| Mwaka | Lengo la Makusanyo (Tsh) | Makusanyo Halisi (TShs.) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 2017/18 | 1,000,000,000 | 1,168,993,197.78 | 117 |
| 2018/19 | 1,000,000,000 | 629,052,950.41 | 63 |
| 2019/20 | 1,000,000,000 | 2,273,544,321.53 | 227.4 |
| 2020/21 | 1,250,000,000 | 6,294,174,783.03 | 504 |
| 2022/23 | 7,488,000,000 | 4,389,810,305.85 | 59 |
| 2023/24 | 6,850,000,000 | 6,180,025,156.38 | 90.2 |
| 2024/25 | 7,000,000,000 | 9,261,668,258.27 | 132.2 |
| JUMLA | 25,588,000,000 | 30,197,268,973.25 | |

**Jedwali : Takwimu za Makusanyo ya Serikali kwa Mwaka 2017/18 hadi 2024/25**

Kutokana na takwimu tajwa hapo juu makusanyo yote ya fedha yaliyopatika kupitia sekta ya madini Mkoa wa Katavi toka mwaka 2021 hadi Juni, 2025 ni Tshs 30,197,268,973.25.

### 9.1.6 Fursa za uwekezaji zilizopo katika Sekta ya Madini

Ili kuvutia wawekezaji wakubwa na wa kati Mkoa umejipanga kutangaza fursa zilizopo katika sekta ya madini. Maeneo muhimu ambayo wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza yamechanganuliwa katika jedwali lifuatalo;

| SN | Aina ya Uwekezaji | Jina la Kijiji | Taratibu za kufuata ili kuanza uwekezaji |
|---|---|---|---|
| 1. | Mitambo ya uyeyushaji wa madini (Smelters) | Eneo lolote ndani ya Mkoa mwekezaji atakalopenda | Mwekezaji afike Ofisi ya Afisa Madini Mkaazi (RMO) –Katavi. |
| 2. | Maghala ya kuuzia baruti (Explosive Mgazine). | Eneo lolote ndani ya Mkoa mwekezaji atakalopenda | Mwekezaji afike Ofisi ya Afisa Madini Mkaazi (RMO) –Katavi. |

## 10.1 SHIRIKA LA VIWANGO (TBS)

### 10.1.1 Idadi ya Watumishi

Kwa mujibu wa ikama watumishi wanaotakiwa katika Ofisi ya Kanda ya Shirika la Viwango (TBS) ni 18 watumishi waliopo ni 10 upungufu ni 8 hii ikiwa ni asilimia 56 ya watumishi waliopo.

### 10.1.2 Utekelezaji wa Shughuli

Kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi mwezi Juni, 2025 idadi ya viwanda vilivyokidhi vigezo na kupata vyeti vya ubora wa bidhaa Mkoa wa Katavi imeongezeka toka 18 mwaka 2021 hadi 44 Juni, 2025. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2025/26 Shirika la Viwango limepanga kutoa vyeti vya ubora wa bidhaa kwa viwanda 10 vitakavyokidhi vigezo vya ubora Mkoani Katavi.

Pia katika kipindi cha mwaka 2022 hadi Juni, 2025 Shirika la Viwango kupitia ofisi ya Kanda ya Magharibi limetoa elimu kwa wadau 202 wa biashara mbalimbali za uchakataji, uzalishaji na ufungashaji wa bidhaa. Mchanganuo wa idadi ya wadau waliopewa mafunzo, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ni wadau 69, Halmashauri ya Wilaya ya Mlele ni wadau 49, Tanganyika wadau 43, Nsimbo wadau 41.

## 11.1 HITIMISHO

Mkoa wa Katavi umejipanga kikamilifu kuvutia wawekezaji na kukuza biashara kwa kuandaa mazingira rafiki kwa wawekezaji na wafanyabiashara ili kuinua uchumi na ustawi wa maendeleo ya Mkoa na Tanzania kwa Ujumla.















**Imeandaliwa na:**
**Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,**
**S.L.P 235,**
**Mpanda - Katavi.**
**Simu Na: +255 25 2957108**
**Fax Na: +255 25 2957108**
**Barua pepe: ras.katavi@tamisemi.go.tz**